

HALMASHAURI YA MJI WA BUNDA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Mji)

MKOA WA MARA

Simu Na. + 255 (028) 2621773
Nakushi Na:+225(028)2621773
Email:td.bunda@mara.go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi,
Halmashauri ya Mji
S.L.P 219,
BUNDA

06 Septemba, 2017.

TANGAZO

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda anayofuraha kutangaza nafasi 2 za kazi ya Afisa Mtendaji wa Kijiji daraja la III yenye ngazi ya mshahara TGS B. Ajira hizo zimetokana na kibali cha Ajira toka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kibali cha Ajira chenye Kumb Na. **CFC.26/205/01*FF*/91** cha tarehe **22/08/2017**.

SIFA ZA MWOMBAJI

1. Awe amehitimu kidato cha nne na awe na astashahada/cheti katika fani zifuatazo:-
 - Usimamizi wa fedha
 - Utawala
 - Maendeleo ya Jamii
 - Sayansi ya Jamii
 - Mipango ya maendeleo vijijini.
 - Sheria
2. Awe na umri usiopungua miaka 18 na si zaidi ya 45.
3. Awe na akili timamu

KAZI NA MAJUKUMU

- (i) Kuratibu na kusimamia upangaji na utekelezaji mipango ya maendeleo ya kijiji.
- (ii) Kusimamia ulinzi na Usalama wa raia na mali zao.
- (iii) Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za Kijiji.
- (iv) Katibu wa Mkutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiji.
- (v) Kusimamia utungaji wa Sheria ndogo za Kijiji.
- (vi) Afisa Masuuli wa Kijiji na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji.
- (vii) Kupokea, kusikiliza na kutatua malalamiko na migogoro ya wananchi.

- (viii) Mwombaji atakapoomba aambatanishe nakala ya Cheti cha kidato cha nne, Astashahada na Cheti cha kuzaliwa.

MASHARTI YA JUMLA

- (1) Waombaji wote wawe raia wa Tanzania.
- (2) Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa
- (3) Waombaji waambatanishe na maelezo binafsi (CV) yenye anuani na namba za simu na majina ya wadhamini.
- (4) Maombi yaambatanishwe na nakala za vyeti vya taaluma na vyeti vya kuhitimu mafunzo ya vyuo.
- (5) Maombi yaambatanishwe na picha moja (passport size) ya hivi karibuni iandikwe jina kwa nyuma.
- (6) Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 20/09/2017.
- (7) Maombi yapelekwe masijala ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Bunda au kutuma kwa anwani ifuatayo:-

Mkurugenzi,
Halmashauri ya Mji,
S.L.P. 219,
BUNDA.

WAOMBAJI WOTE MNAKARIBISHWA

J. Mayanja
Janeth P. Mayanja
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI
BUNDA